**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA**
(*Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa*)

***Unapojibu tafadhali taja:***

**Kumb.Na.BMC/S.35/49/79** **24/05/2022**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi ya nafasi za kazi kama ifuatavyo:

### 1. KATIBU MAHSUSI III - NAFASI 4

**A: SIFA ZA MWOMBAJI:**

i) Aliyefaulu elimu ya Kidato cha nne (IV)
ii) Awe na Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu.
iii) Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza Maneno 80 kwa dakika moja.
iv) Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali, na kupata cheti katika Programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail, na Publisher.

**B: MAJUKUMU YA KATIBU MAHSUSI III:**

i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
ii) Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
iii) Kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi,wageni,tarehe za vikao,safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
iv) Kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka na kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.

v) Kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.

vi) Kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

vii) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

**C. MSHAHARA**

Cheo cha Katibu Mahususi Daraja la III kina mshahara wa **TGS B** kwa mwezi.

**2. DEREVA DARAJA LA II - NAFASI 4**

**A: SIFA ZA MWOMBAJI:**

i) Aliyefaulu elimu ya Kidato cha nne (IV)

ii) Awe na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali

iii) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali

iv) Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

**B: MAJUKUMU YA DEREVA DARAJ LA II:**

i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari

ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi

iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya magari

iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali

v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari za safari

vi) Kufanya usafi wa magari , na

vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

**C. MSHAHARA**

Cheo cha Katibu Mahususi Daraja la III kina mshahara wa **TGS B** kwa mwezi.

## 3. MHUDUMU WA JIKONI DARAJA LA II - NAFASI 2

### A: SIFA ZA MWOMBAJI:

i) Aliyefaulu elimu ya Kidato cha nne (IV)

ii) Awe na uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu

### B: MAJUKUMU YA MHUDUMU WA JIKONI DARAJA LA II

i) Kusafisha vyombo vya kupikia

ii) Kusafisha vyombo vya kulia chakula

iii) Kusafisha meza itumiwayo kwa kulia chakula

iv) Kuwatayarishia wapishi/Waandazi vifaa vya mapishi na Mezani

v) Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia

vi) Kuwasaidia Waandazi na Wapishi

### C. MSHAHARA

Cheo cha Mhudumu wa Jikoni Daraja la II kina mshahara wa **TGOS A** kwa mwezi.

### MASHARTI YA JUMLA

i) Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania

ii) Waombaji wote wawe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

iii) Waombaji wote wawe hawajawahi kupatikana na kosa la jinai, kugushi vyeti au kufungwa jela.

iv) Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) watatu wa kuaminka pamoja na namba zao za simu.

v) Waombaji wote waambatishe nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha 1 (passport size) ya hivi karibuni iliyoandikwa jina la mwombaji nyuma.

vi) Waombaji wote waambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA

vii) Testimonials "Transcripts", "Provisional Results", "Statement of results", na "Result Slips" hazitakubaliwa.

viii) Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganifu na NECTA, NACTE na TCU

ix) Mwisho wa kuleta maombi ni tarehe **06/06/2022 saa 9:30** mchana.

x) Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa:-

**MKURUGENZI WA MANISPAA,**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA,**
**S.L.P.284,**
**BUKOBA.**

Dkt. Mustafa M. Waziri
**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA**
**BUKOBA**

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
BUKOBA

**Nakala: " Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira,**
**www.ajira.go.tz**
**" Tovuti ya Halmashauri,**
**www.bukobamc.go.tz**
**"Mbao za Matangazo**